



OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI



WIKI HII MAGAZETINI NA MITANDAONI

19/05/2025 ► 24/05/2025

OAG

jijini Dra es Salaam. (Na Mpigapicha Wetu)

Kamati ya ushauri wa kisheria na kliniki bila malipo yazinduliwa Singida

Na Mwandishi Wetu

■■■ OFISI ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkoo wa Mkoa wa Singida imezindua rasmi Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria bila malipo kwa wananchi wa Mkoa wa Singida. Uzinduzi huo ulifanyika juzi katika viwanja vya Stendi ya zamani Mansipaa ya Singida.

Akizungumza katika uzinduzi huo, mgeni rasmi na Mkoo wa Mkoa wa Singida Halima Dendego alipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa kuuchagua Mkoa wa Singida na kuja kuzindua Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya kwa kuwa ni fursa kwa wananchi wa mkoa huo kutatuliwa changamoto mbalimbali za kisheria zinazowakabili.

"Kipekee naishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali na Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya kwa kunifikiria na kunipa wajibu huu mkubwa wa kuwa Mgeni Rasmi katika Halfa hii ya Uzinduzi wa Kamati na Kliniki ya Sheria bila malipo katika mkoa wetu" alisema Dendego.

Dendego alisema kuwa kuzinduliwa kwa Kamati hiyo pamoja na masuala mengine, kutasaidia Kupunguza mashauri au migogoro dhidi ya Serikali, kuwawezesha Mawakili wa Serikali kusimamia Utawala wa Sheria katika maeneo yao, Kuwawezesha Mawakili wa Serikali kushirikiana na wadau wengine katika kutatua kero za wananchi na kupunguza malalamiko ya kisheria kutoka kwa wananchi.

"Naomba kukuahidi Mwanasheria Mkoo wa Serikali kuwa nitazisimamia Kamati hizi kikamilifu ili ziweze kuwa na tija katika mkoa wetu." alisema Dendego

Katia hatua nyingine Mkoo wa Mkoa wa Singida ametoa wito kwa Wananchi wa Mkoa huo kujitokeza kwa wingi katika Kliniki ya Sheria bila malipo ili waweze kupata huduma mbalimbali za kisheria hususani katika masuala ya mirathi, Ardhi, ndoa na Ajira.

"Nitoe wito kwa Wananchi wa Singida kujitokeza kwa wingi katika Kliniki hii kwani Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali imekuja na Watalamu waliobobeza katika masuala ya Kisheria na wanatoa huduma hii bure kabisa" alisema Dendego

Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Hamza S. Johari alisema kuwa kuzinduliwa kwa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya pamoja na Kliniki ya Sheria kwa Wananchi wa Mkoa wa Singida ni mojawapo ya hatua za Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali katika kusogeza huduma za kisheria karibu zaidi na wananchi.

Aidha, Mwanasheria Mkoo wa Serikali alieleza kuwa moja ya njia inayotumiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kuwajibika kwa wananchi ni kutoa ushauri na msaada wa kisheria kwa wananchi kwa kutumia Kamati za Ushauri wa Kisheria kwa ngazi ya Mkoa na ngazi za Wilaya.

"Lengo kuu la uanzishwaji wa Kamati za Ushauri wa Kisheria kwa ngazi ya Mkoa na Wilaya ni kurahisisha usimamizi wa utoaji wa ushauri wa kisheria kwa wananchi katika maeneo husika" alisema

Mwanasheria Mkoo wa Serikali.

Mwanasheria Mkoo wa Serikali amesema kuwa, Uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria kwa Mkoa wa Singida utafutiwa na Kliniki ya sheria kuanzia tarehe 19 hadi 25 Mei, 2025 ambapo huduma za ushauri wa kisheria zitatolewa kwa wananchi bila malipo, ambapo amesitiza Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali itatoa huduma hizo kwa ubora.

"Tunawaahidi tutatoa huduma hii bila malipo kwa wananchi na kwa weledi mkubwa" alisema Mwanasheria Mkoo wa Serikali

Vilevile, Mhe. Johari amesema kuwa Kliniki hiyo ya Sheria inalenga kusogeza huduma za sheria karibu na wananchi, kuwaongoza wananchi katika taratibu za kupata haki zao pale zinapovunjwa au zinapoonekana kuelekeea kuvunjwa, kutoa elimu ya sheria kwa wananchi na kuongeza ushirikiano mionganoni mwa Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea, na kuepusha au kupunguza mashauri yasiyo ya lazima.

"Kupitia huduma zitakazotolewa kwenye Kliniki hii ya Sheria tunaamini tutaongeza utengamano na utulivu katika jamii, kudumisha utawala bora kwa kuimarisha utawala wa sheria nchini, na kuchocha maendeleo kwa jamii na taifa kwa ujumla" alisema Johari.

Kliniki ya Sheria Bila malipo kwa Wananchi wa Mkoa wa Singida imezinduliwa tarehe 19 Mei na itaendelea kutoa huduma za kisheria kwa Wananchi wa Mkoa wa Singida hadi tarehe 25 Mei, 2025 katika Viwanja vya Stendi ya zamani Mansipaa ya Singida.

Mawakili wa Serikali watakiwa kujitoa kwa moyo

Na Jumbe Ismailly, Singida

MWANASHERIA Mkuu wa serikali, Hamza Saldi Johari amewataka Mawakili wa serikali kujitoa kwa moyo katika kusikiliza malalamiko na kuyatafutia suluhukwa weledi pamoja na umahiri mkuuwa.

Akitoa wito huo wakati wa wa uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na wilaya na Kliniki ya sheria bila malipo uliofanyika kwenye viwanja vya kituo cha zamani cha mabasi kilichopo Kata ya Majengo, Manispaa ya Singida, Mwanasheria huyo alifafanua kwamba mawakili hao kwa nafasi zao pia ni viongozi au wajumbe wa kamati ya ushauri wa kisheria ngazi ya Mkoa na wilaya na kliniki ya sheria bila malipo.

Aidha Mwanasheria Hamza alizitaka pia kamati za ushauri wa kisheria za mikoa na wilaya kufuatilia na kutatua changamoto zote zinazoibuliwa wakati wa kampeni wa msaada wa kisheria ya Mama Samia.

Hata hivyo Mwanasheria huyo Mkoo wa serikali alitumia fursa hiyo kwa kuwataka wananchi kuzitumia kamati hizo ambazo zitakuwa karibu nao katika mikoa na wilaya zao kwani kamati hizo zimepewa jukumu la kupokea na kutafuta suluhisho la changamoto mbali mbali za kisheria zinazowakabilii wananchi.

â€œKwa mikoa na wilaya ambazo bado hazijakamilisha uundwaji wa kamati hizo, wajitahidi kukamilisha zoezi hilo mapema, ofisi yangu itatoa ushirikiano wa kutosha katika kufanikisha kukamilika kwa zoezi hilo ili huduma hizi za ushauri wa kisheria kwa wananchi bila malipo ziweze kuwafikia wananchi wa mikoa na wilaya hizo piaâ€ alisitisiza Hamza ambaye ni mwanasheria mkuu wa serikali.

Akizindua kamati hiyo ya ushauri wa kisheria ngazi ya Mkoa na wilaya na kliniki ya sheria bila malipo mkoani Singida, Mkoo wa mikoa wa Singida, Halima Omari Dendego alielekeza kamati ya ushauri huongazi

ya mkoa, wilaya pamoja na wadau kuendelea kushirikiana na serikali katika kuwashudumia wananchi, ikiwa ni pamoja na kutatua migogoro na kero za wananchi wa Singida.

â€œOfisi ya Mwanasheria Mkoo wa serikali na kamati za ushauri wa kisheria kwa kushirikiana na ofisi yangu, zimeonyesha mfano mzuri wa ushirikiano kwa kutoa huduma za ushauri wa kisheria ndani ya Mkoa wa Singida kwa kuandaa kliniki ya sheria itakayofanyika hapa kwa juma zimaâ€ alifafanua Dendego huku akishangiliwa na kikundi cha wanawake wa Mama Samia.

Hata hivyo mkoo huyo wa Mkoa aliwahakikisha wananchi wa Mkoa wa Singida kwamba serikali kuitopia ofisi yake itaendelea kuweka mazingira wezeshi katika utatuzi wa migogoro na kero za wananchi wa Mkoa wa Singida.

Akizungumza kwa niabayaviongozi wakimilawa Mkoa wa Singida, Kiongozi wa Machifu, Mughenyi Senge pamoja na kuipongeza serikali ya awamu

ya sita kwa kupeleka huduma hiyo lakini alionesha kutoridhishwa na jinsi wananchi wanavyodhulumiwa haki zao kwenye kitengo cha sektaya Ardhi.

Alisitisiza kiongozi huyo wa kimila kwamba viongozi wa kimila wamekuwa wakipokea malalamiko mengi yahusuyo migogoro ya ardhilakini kutokana na kutokuwa na uwezo wa kuitatua na kuitolemaamuzi wamekuwawakitumia kauli za kukemea wale wanaotuhumiwa jambo ambalo kwa namna moja au nyiningine halitawezza kumaliza migogoro ya kitengo hicho cha ardhil.

Kwa upande wake Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kyaratu aliweka bayana kwamba bado kuna tatzizo kubwa la upatikanaji wa huduma za kisheria linalochangiwa na gharama kubwa zinazotozwa na wanasheria, jambo ambalo huchangia idadi kubwa ya wananchi kupoteza haki zao kutokana na kutopata sehemu zinakopatikana huduma hizo kwa njia za bure.

AG awafunda mawakili wa serikali

Na Thobias Mwanakatwe,
SINGIDA

MWANASHERI Mkuu wa Serikali (AG), Hamza Johari (pichani), amewataka mawakili wa serikali kusikiliza na kutafuta suluhu kwa weledi za malalamiko ya wananchi ili kuendeleza utawala wa sheria nchini.

Johari, alitoa rai hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya mkoa na wilaya mkoani hapa ulioambatana na Kliniki ya Sheria uliofanyika viwanja vya stendi ya zamani mjini hapa.

Alisema ili kudumisha amani na utengamano na kuchochea maendeleo kwa Jamii na taifa, wananchi wanapaswa kusikilizwa na kutatuliwa changamoto zinazowakabili.

"Moja ya njia inayotumiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwajibika kwa wananchi

ni kutoa ushauri wa kisheria kwa ngazi ya mkoa na wilaya ndio maana mwongozo ultolewa wa uanzishwaji kamati za ushauri wa kisheria za mkoa na wilaya," alisema Johari.

Alisema lengo kuanzishwa kwa kamati hizo ni kurahisisha usimamizi wa utoaji wa ushauri wa kisheria kwa wananchi katika maeneo yao.

Akizungumzia kuhusu kliniki za kisheria, alisema zimelen-ga kuwaongoza wananchi katika taratibu za kupata haki zao pale zinapovun-jwa au zinapoonekana kuelekeea kuvunjwa.

Akizindua kamati hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema itasaidia k u p u n g u z a mashauri na m i g o g o r o dhidi ya wananchi na serikali.

Dendego, alisema kama-ti hizo pia zitawawezesha mawakili wa serikali kusima-mia utawala wa sheria katika maeneo yao, kushirikiana na wadau kutatua kero za wananchi na kupunguza makala-miko yao ya kisheria.

"Naomba kukuahidi Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa nitazisimamia kamati hizi kikamilifu ili ziweze kuwa na tija katika mkoa wetu," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi mkoani hapa kujitokeza kwa wingi katika Kliniki ya Sheria bila malipo ili waweze kupata huduma za mirathi, ardhi, ndoa na ajira.



Ijumaa Mei 23, 2025

Nipashe 15

HABARI DODOMA



Migogoro ya ardhi, ndoa yashamiri Singida

Na Thobias Mwanakatwe,
SINGIDA

WANASHERIA wabobezi walikweli kambi mkoani Singida kwa ajili ya kuendesha kliniki ya sheria, wamebalini changamoto kubwa zisazowakabili wananchi wa mkoani huu na migogoro ya ardhi, ndoa, ajira na masuala ya kijinsia.

Wanasheria hao-kutoka ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Sheria na Katiba wameweka kambi ya siku tano mikounda Singida iliyosanzu Mei 19 na itabitimishwa Mei 25 mwaka huu kwa ajili ya kuwasaidia wananchi masuala mbalimbali ya kisheria.

Mkarugenzi wa Divisieri ya Uratibu na Huduma za Ushauri

ri wa Kisheria, Neema Ringo, akizungumza jana alisema wananchi wengi wameendelea kujitokeza kupata mesaada wa kisheria katika mbaro mbalimbali yanayowakabili.

Ringi alitoa wito kwa wananchi waendelea kujitokeza zaidi katika kliniki hiyo ili waweze kiaipa ushauri wa kisheria imyotolewa na Ofisi ya Mwanasheria

Mkuu wa Serikali kwa wananchi wa Singida bila malipo.

Mwananchi mwininge Engeridji Makala aliushuruki uongozwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuleta huduma hiyo ya kisheria mkoani Singida.

Wakati wa kufungua kliniki hiyo juzi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, amewataka mawakili wa serikali kusikiliza na

kutafuta suluhu kwa weledi malalamiko yanayobusu masuala ya kisheria ambayo yanawakabili wananchi ili kuendeleza utawala wa sheria nchini.

Alisema ili kudumisha amani na utengamano na kuchochea maendeleo kwa Jamii na taifa wananchi wanapaswa kusikilizwa na kutatuliwa changamoto zao na serikali.

Mawakili wa serikali watakiwa kujitua kutatua malalamiko ya wananchi

NA JUMBE ISMAILY, SINGIDA

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Saidi Johari amewataka mawakili wa serikali kujitua kwa moyo katika kusikiliza malalamiko na kuyatafutia suluhi kwa weledi.

Alitoa wito huo wakati wa wa uzinduzi wa kamati ya ushauri wa kisheria ngazi ya mkoa na wilaya na kliniki ya sheria bila malipo, uliofanyika viwanja vyta cha zamani cha mabasi kilichopo Majengo, manispaa ya Singida.

Alisema mawakili hao kwa nafasi zao pia ni viongozi au wajumbe wa kamati ya ushauri wa kisheria ngazi ya mkoa na wilaya na kliniki ya sheria bila malipo.

Aidha alizitaka pia kamati za ushauri wa kisheria za mikoa na wilaya kufuatalia na kutatua changamoto zote zinazoibuliwa

wakati wa kampani wa msaada wa kisheria ya mama Samia.

Alitumia fursa hiyo kuwaomba wananchi kuzitumia kamati hizo kutatua changamoto zinazowakabili.

Mkuu wa mkoa wa Singida, Halima Omari Dendego, alizitaka kamati hizo na wadau kuendelea kushirikiana na serikali katika kuwahudumia wananchi.

"Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali na kamati za ushauri wa kisheria kwa kushirikiana na ofisi yangu, zimeonyesha mfano mzuri wa ushirikiano kwa kutoa huduma za ushauri wa kisheria ndani ya mkoa wa Singida kwa kuandaa kliniki ya sheria itakayofanyika hapa kwa juma zima," alifanua.

Aliwahakikishia wananchi kwamba ofisi yake itaendelea kuweka mazingira wezeshi katika utatuzi wa migogoro na kero zao.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi wa kimila wa mkoa wa Singida, Kiongozi wa Machifu, Mughenyi Senge, alieleza kutoridhishwa na jinsi wananchi wanavyodhulumiwa haki zao kwenye kitengo cha sekta ya ardhi.

Alisema viongozi wa kimila wana pokea malalamiko mengi yahusuyo migogoro ya ardhi lakini kutokana na kutokuwa na uwezo wa kuitatua na kuitolea maamuzi, wanakemea wale wanaotuhumiwa kuwa chanzo.

Mstahiki Meya wa manispaa ya Singida, Yagi Kyaratu alisema bado kuna tatizo la upatikanaji wa huduma za kisheria linalochangiwa na gharama kubwa zinazotozwa na wanasheria, jambo ambalo huchangia idadi kubwa ya wananchi kupoteza haki zao.

[Home](#) > [Habari](#)

Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali yabisha hodi Singida

SINGIDA-Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkoo wa Mkoa wa Singida imezindua rasmi Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria bila malipo kwa wananchi wa Mkoa wa Singida.



Uzinduzi huo umefanyika tarehe 19 Mei, 2025 katika viwanja ya Stendi ya zamani Manispaa ya Singida.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mgeni Rasmi na Mkoo wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima O. Dendego ameipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa kuuchagua Mkoa wa Singida na kuja kuzindua Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya kwa kuwa ni fursa kwa wananchi wa mkoa huo kutatuliwa changamoto mbalimbali za kisheria zinazowakabili.

05



Responsive Advertisor

HOME HABARI MICHEZO MAKALA SIASA VIDEO MAGAZETI YOUTUBE CHANNEL

BREAKING NEWS SMAUJATA SINGIDA WATOA POLE KWA MAFURIKO NA AJALI YA GARI

Home > HABARI

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AWAPA HABARI NJEMA YA KISHERIA SINGIDA

By Amini Nyaung'o | May 10, 2025

0

Na Amini Nyaung'o



Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza Johari amesema kuwa jopo la wanasheria waliofika Mkoani Singida watasaidia wananchi mbalimbali watakaokuwa na shidaa za kisheria kwa siku saba ambapo leo ndio ulikuwa uzinduzi wake Stendi ya zamani Mkoani Singida.

Hayo ameyasema leo katika uzinduzi wa Kisheria uliofanyika Stendi ya zamani ya Mabasi Mkoani hapa.

06



oagtanzania



www.oag.go.tz

MITANDAONI

19/05/2025



OAG Tanzania

4d ·

MATUKIO KATIKA PICHA

Uzinduzi wa Kamati ya Kudumu ya Ushauri wa Kisheria Ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria ya bola malipo kwa Wananchi wa Mkoa wa Singida.

Like

Comment

Send

Share



[oagtanzania](#)



www.oag.go.tz

MITANDAO NI 19/05/2025



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI



MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKITOA HUDUMA YA USHAURI WA KISHERIA

Tarehe 19 Mei, 2025.

#Singidalumewafikia
#Klinikiyasheribilamalipo

✉ info@oag.go.tz ☎ Tel 0800110188 📺 @oagtanzania 🌐 www.oag.go.tz

Nyumbani > WANANCHI WAIPA TANO OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KWA HUDUMA YA KILINIKI YA KISHERIA SINGIDA.

WANANCHI WAIPA TANO OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KWA HUDUMA YA KILINIKI YA KISHERIA SINGIDA.

Na Mwanahabari wetu Singida.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kusogeza huduma za kisheria kwa wananchi ambapo Ofisi inafanya Kliniki ya Sheria bila malipo kwa Wananchi wa Mkoa wa Singida.

Akizungumza wakati wa Kliniki hiyo Mkurugenzi wa Divisheni ya Uratibu na Huduma za Ushauri wa Kisheria, Bi. Neema Ringo ameridhishwa na mwitikio wa wananchi wanaojitokeza kupata huduma mbalimbali katika kliniki hiyo, ambapo ameelleza kuwa masuala ya ajira, ardhi, ndoa na masuala ya kijinsia yamekuwa ni changamoto kwa wananchi wengi waliojitekeza katika kliniki hiyo.



Wananchi wamiminika kliniki ya sheria bila malipo Singida

Yasini Ngatu · 3 days ago

2 minutes read



Facebook



X



Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kusogeza huduma za kisheria kwa wananchi ambapo Ofisi inafanya Kliniki ya Sheria bila malipo kwa Wananchi wa Mkoa wa Singida ilyoanza tarehe 19 na inaendelea hadi tarehe 25 Mei, 2025 katika viwanja vya Stendi ya zamani Manispaa ya Singida.

Akizungumza wakati wa Kliniki hiyo Mkurugenzi wa Divisheni ya Uratibu na Huduma za Ushauri wa Kisheria, Neema Ringo ameridhishwa na mwitikio wa wananchi wanaojitokeza kupata huduma mbalimbali katika kliniki hiyo, ambapo ameeleza kuwa masuala ya ajira, ardhi, ndoa na masuala ya kijinsia yamekuwa ni changamoto kwa wananchi wengi waliojitekeza katika kliniki hiyo.



oagtanzania

⋮



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI



**Uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa
Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya
na Kliniki ya Sheria bila malipo
Mkoa wa Singida.**

Ni Leo

Siku: **Jumatatu**

Tarehe: **19 Mei, 2025**

Mahali: Viwanja vya Stendi ya zamani
Manispaa ya Singida

#Singidalumewafikia

wote mnakaribishwa!

info@oag.go.tz

Tel 0800110188



@oagtanzania

www.oag.go.tz

View insights

Boost post



8



Liked by mangununu and others

11



oagtanzania



www.oag.go.tz



oagtanzania

⋮



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI



**Zimebaki
Siku**

2

Tarehe **25 Mei, 2025** ni Siku ya
Mwisho ya Kliniki ya Sheria bila
malipo kwa wananchi wa mkoa
wa Singida

Wahi sasa katika Viwanja vya Stendi
ya zamani Manispaa ya Singida
tukuhudumie

#Singidalumewafilia

info@oag.go.tz Tel 0800110188 @oagtanzania www.oag.go.tz



TUPO KARIBU YAKO!

Tufuatilie kupitia ✅



[oagtanzania](#)



info@oag.go.tz



www.oag.go.tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mitumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania

KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188

Weledi na Ubora